

TANGAZO LA SERIKALI NA. 215 la tarehe 12/10/2007

**SHERIA YA VYAMA VYA SIASA
(SURA YA 258)**

KANUNI

(Zimetungwa chini ya fungu la 22(h))

**KANUNI ZA MAADILI YA VYAMA VYA SIASA ZA
MWAKA 2007**

**SEHEMU YA KWANZA
UTANGULIZI**

la Kanuni

1. Kanuni hizi zitaitwa Kanuni za Maadili ya Vyama vya Siasa

Mwaka 2007 na zitaanza kutumika mara tu baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

tumizi

2. Kanuni hizi, zitatumika Tanzania Bara na vile vile Tanzania Zanzibar.

fanuzi

3. Katika Kanuni hizi, isipokuwa pale muktadha utaelekeza vinginevyo-
"chama cha siasa" maana yake ni chama cha siasa chenye usajili wa kudumu kwa mujibu wa Sheria.

"Msajili" maana yake ni Msajili wa Vyama vya Siasa aliyeteuliwa kwa mujibu wa kifungu cha 4 cha Sheria pia itajumuisha Naibu Msajili na Msajili Msaidizi;

ya

“Sheria” maana yake ni Sheria ya Vyama vya Siasa.

SEHEMU YA PILI HAKI YA CHAMA

ki za Vyama
Siasa

4.-(1) Kila chama cha siasa kitakuwa na haki zifuatazo-

- (a) Kutoa elimu ya uraia na elimu ya uchaguzi kwa wananchi kwa kufuata sheria na kanuni za nchi;
- (b) Kutoa maoni ya kisiasa kadiri itakavyoona inafaa ili kutekeleza sera zake, kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba ya Zanzibar;
- (c) Kujadili na kushindanisha sera zake na zile za chama cha siasa kingine kwa lengo la kutaka kukubalika na wananchi;
- (d) Kuwa na uhuru wa kutafuta wanachama na kama ni wakati wa kampeni basi kuwe na uhuru wa kutafuta kuungwa mkono na wapiga kura; na
- (e) Kila chama cha siasa kitakuwa na haki ya kufanya mikutano ya kisiasa na maandamano kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa;

(2) Wakati wa uchaguzi wowote utakaoendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi, kila chama cha siasa kitakuwa na haki na uhuru wa kushiriki na kushirikishwa na Tume ya Uchaguzi na au chombo chochote chenye mamlaka katika kufanya uchunguzi na kupata matokeo katika jambo au suala lolote linalohusu uchaguzi.

SEHEMU YA TATU WAJIBU WA CHAMA

Wajibu wa
vyama vya siasa

5.-(1) Kila chama cha siasa kitakuwa na wajibu wa kutunza maadili chini ya kanuni hizi kwa:-

- (a) kuzieleza kwa wanachama wake ili kuongeza uadilifu wa kisiasa ndani na nje ya chama cha siasa;
- (b) kulaani, kuepukana kuchukua hatua zitakazofaa ili kuzuia au kuepusha vitendo vya vurugu, uvunjaji wa amani au ukandamizaji wa aina yoyote ile;
- (c) kutotumia vyombo vya dola kukandamiza na kutoa vitisho kwa chama cha siasa kingine kwa manufaa yake;
- (d) kutotoa maneno yoyote au maandishi ambayo ni ya uongo kuhusu mtu yoyote au chama cha siasa chochote;
- (e) kufanya mkutano wa kisiasa na maandamano bila kufanya vurugu kwa mujibu wa sheria za nchi;
- (f) kulaani na kupinga -
 - (i) vitendo vyenye kuashiria ukandamizaji;
 - (ii) matumizi ya lugha ya matusi
 - (iii) vitendo vya kibabe na vurugu;
 - (iv) matumizi ya nguvu ili kujipatia umaarufu wa chama au sababu yoyote ile;
- (g) kuepuka kuteremsha bendera iliyowekwa kwa mujibu wa Sheria, kuharibu kwa namna yoyote ile kitu chochote ambacho ni ishara au nembo inayotumiwa na chama kingine kama sehemu ya utambulisho wa chama hicho;
- (h) kuepuka kushawishi kwa kutoa rushwa kama kichocheo ili kupata upendeleo au heshima kwa nia ya kufanikisha malengo;
- (i) kuepuka kutumia mamlaka, rasilimali za serikali, vyombo vya dola, au wadhifa wa kiserikali, kisiasa au ufadhili wa nje ama wa ndani kwa namna yoyote ile ili kukandamiza chama kingine;
- (j) kuepuka vitendo vya ubaguzi wa rika, kabila, jinsia, dini na mahali alipozaliwa mtu yeyote ikiwa ni jamii au asili fulani kwa kufanikisha malengo ya siasa; na
- (k) kuheshimu maamuzi halali yaliyofanywa kwa pamoja na vyama vyote.

(2) Kwa kuzingatia Sheria, kila chama cha siasa kitakuwa na uhuru wa kushirikiana na chama cha siasa kingine kwa nia njema kwa ajili ya kupanga vikao, mikutano ya hadhara kwa pamoja au maandamano kwa wakati mmoja kama kwamba mambo hayo yamefanywa na chama cha siasa kimoja au bila kuvunja sheria za nchi.

**SEHEMU YA NNE
WAJIBU WA MSAJILI**

Wajibu wa
Msajili

6.-(1) Ili kuhakikisha kwamba Kanuni hizi zinatekelezwa, Msajili atakuwa na wajibu wa –

- (a) kusimamia madili ya vyama vya siasa;
- (b) kupokea malalamiko yaliyowasilishwa kwake yanayohusu ukiukwaji wa maadili haya na kusikiliza pande zote;
- (c) kuzuia kitendo cha uvunjifu wa Kanuni za maadili kisiendeleo na kukitaka chama au kumtaka kiongozi wa chama kujirekebisha; na
- (d) kutoa onyo la maandishi kwa chama au kiongozi wa chama husika.

(2) Iwapo baada ya kutolewa onyo la kwanza kwa mujibu wa Kanuni (1)(d), chama cha siasa kitaendelea au kiongozi ataendelea kukiuka maadili hayo, Msajili atakemea hadharani ukiukwaji huo wa maadili

Malalamiko ya
uvunjwaji wa
maadili

7.-(1) Bila ya kuathiri masharti ya Kanuni ya 5, malalamiko dhidi ya uvunjwaji au ukiukwaji wa maadili yatapelekwa kwa maandishi kwa mtu yeyote kwa maandishi yakiwa yamesainiwa na mlalamikaji.

(2) Mara baada ya kupokea malalamiko, Msajili ataanza kufanya Uchunguzi dhidi ya chama cha siasa kinacholalamikiwa.

Imesainiwa na,

Dar es Salaam
1 Oktoba, 2007

EDWARD N. LOWASSA
Waziri Mkuu